

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



MKUU WA TAKUKURU MKOA
Mtaa wa Uzunguni,
S.L.P 37,
37101 SHINYANGA,
Tanzania.
Simu: (028) 2762630
Nukushi: (028) 2763358

01 Julai 2020.

TAARIFA KWA UMMA.

**TAKUKURU KAHAMA YAOKOA SHILINGI MILIONI KUMI NA TANO ZA WALIMU
WASTAAFU NA UJENZI WA KITUO CHA AFYA NGAYA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA.**

Ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Shinyanga inaendelea na uchunguzi wa ubadhirifu wa fedha katika Chama cha Akiba na Mikopo cha Walimu Kahama (WALIMU KAHAMA SACCOS LTD). Fedha hizi kiasi cha Sh. 7,780,625/= zilizookolewa zitalipwa moja kwa moja kwa Walimu Wastaafu wanaokidai Chama Cha Akiba na Mikopo cha Walimu Kahama (WALIMU KAHAMA SACCOS LTD) na Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mhe. Anamringi Macha.

Aidha katika uchunguzi uliofanyika kuhusiana na ujenzi wa Kituo cha Afya cha NGAYA kilichopo kata ya NGAYA Halmashauri ya Msalala, Ofisi ya TAKUKURU (W) Kahama imefanikiwa kuokoa kiasi cha **shilingi 7,275,500/=** ambazo zitakabidhiwa leo na Mkuu wa Wilaya ya Kahama Mhe. Anamringi Macha kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya MSALALA Ndugu. Simon Berege.

Kwa hiyo jumla ya fedha zilizookolewa na ambazo zitalipwa kwa walimu wastaafu na kukabidhiwa Halmashauri (W) Msalala ni **sh. 15,056,125.00.**

DENI LA WALIMU WASTAAFU.

Uchunguzi uliofanyika na TAKUKURU mkoa wa Shinyanga kwa WALIMU KAHAMA SACCOS LTD umebaini kwamba chama hiki kinadaiwa na walimu wastaafu **ishirini na tisa (29)** jumla ya **sh. 13,396,425.00.** Deni hili linatokana na akiba za walimu wastaafu walizokuwa wanachangia wakati wakiwa kazini baada ya kustaafu akiba hizi hazikuweza kupatikana kwa kuwa chama kilikuwa hakina fedha.

Awamu ya kwanza ofisi ya TAKUKURU (W) Kahama iliokoa jumla ya **sh. 5,815,800.00**, fedha hizi zililipwa kwa walimu wastaafu kumi na tatu (**13**) waliokuwa wanakidai Chama cha Akiba na Mikopo cha Walimu Kahama SACCOS.

Katika awamu hii ya pili Ofisi ya TAKUKURU (W) Kahama imefanikiwa kuokoa kiasi cha **sh. 7,780,625.00** fedha ambazo zitalipwa kwa walimu wastaafu **kumi na sita (16)** waliosalia ambao walikuwa wanchama wa WALIMU KAHAMA SACCOS LTD.

FEDHA ZA UJENZI WA KITUO CHA AFYA NGAYA ZILIZOOKOLEWA SH. 7,275,500/=

TAKUKURU Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga ilifanya uchunguzi kuhusiana na ujenzi wa Kituo cha Afya cha NGAYA kilichoko kata ya NGAYA Halmashauri ya Msalala ambapo katika uchunguzi huo ilibainika kuwa kiasi cha **sh. 7,275,500/=** kimepotea kutokana na Mtaalamu kitengo cha manunuzi kutotekeleza majukumu yake ipasavyo; hivyo ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Kahama kwa kushirikiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Msalala, imefanikiwa kuokoa fedha hizo. Kwa kuwa kuna kazi ambazo hazijakamilika za ujenzi wa zahanati hiyo, fedha hizo zitakabidhiwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala.

WITO.

TAKUKURU (M) SHINYANGA inatoa wito kwa watumishi wa umma mkoani humu kufanya kazi kwa weledi, uadilifu, uzalendo, uaminifu na kwa kufuata sheria zote za nchi ili fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali zitumike kama ilivyokusudiwa. **Iwapo mtumishi wa umma (mtaalam) atashindwa kuwajibika ipasavyo na hivyo kusababisha upotevu wa fedha ya Serikali mtumishi huyo atarejesha fedha iliyopotea na hatua nyingine za kisheria zitafuata ikiwemo ya kumfikisha mahakamani.**

Aidha TAKUKURU mkoa wa Shinyanga inatoa wito kwa Watumishi wa Umama mkoani humu kufichua vitendo vya rushwa vinavyotokea katika maeneo yao ya kazi. Wapo watumishi wananwake ambao wanaombwa rushwa ya ngono ili waweze kupatiwa upendeleo mfano kupandishwa cheo, kupatiwa uhamisho, kupatiwa ruhusa ya kwenda masomoni na huduma nyingine zinazofanana na hizo. TAKUKURU (M) SHINYANGA inatoa wito kwa watumishi wanaokutana na vitendo hivi kutoa taarifa ili wahusika wachukuliwe hatua mara moja.

Imetolewa leo tarehe 02/07/2020 na Mkuu wa TAKUKURU (W) Kahama Kwa Niaba ya Mkuu wa TAKUKURU mkoa wa Shinyanga.